

## **UJENZI WA MRADI WA SKIMU YA UMWAGILIAJI BWAWA LA INALA**

Mradi wa Skimu ya umwagiliaji Inala ni mradi ulioanzishwa na Kujengwa katika Kijij cha Inala kata ya Ndevelwa ambaa umehusisha ujenzi wa Bwawa na Miundo mbinu ya Umwagiliaji ambapo hadi sasa bwawa lina ujazo wa mita za ujazo 1,376,000 ambalo lina uwezo wa kumwagilia eneo la ukubwa wa hekta 400 wakati wote kwa ajili ya kilimo cha mpunga , mahindi na mboga mboga.

Vilevile Halmashauri imefanikiwa kujenga miundo mbinu ya umwagiliaji kufikia hekta 232 na gharama ya mradi huu kwa ujumla ni Tsh. 1,656,342,651.809 ikihusisha ujenzi wa bwawa pamoja na skimu ya umwagiliaji.

Mradi ulianzishwa kwa lengo la kutatua changamoto ya ukosefu au upungufu wa Chakula kwa wakazi wa Manispaa ya Tabora ambaa husababishwa na kilimo duni kutokana na Manispaa ya Tabora kutopata mvua za kutosha kuwezesha shughuli za kilimo cha mazao ya chakula kama mpunga na mahindi hivy kuisababishia serikali gharama kubwa ya kutoa chakula cha msaada ili kuokoa kaya ambazo huathirika kutokana na ukosefu wa chakula

Mafanikio ya mradi ni kwamba sasa wakulima wapatao 400 wamegawiwa mashamba ili kuanza kilimo cha mpunga na inatarajiwa ujenzi wa skimu ukikamilika wakulima wapatao 1000 watanufaika kwa kulima kilimo chenye tija na kupata uhakika wa chakula , kuinua kipato cha wakulima, kukua kwa uchumi katika Manispaa na wakulima waliopo karibu na mradi kupata maji ya kunyweshea mifugo yao.

Wakulima wamepatiwa mafunzo kuitia mashamba darasa yaliyotolewa na Wataalamu kutoka Manispaa ya Tabora kwa Kushirikiana na Wataalamu kutoka Chuo cha Kilimo Tumbi

## **Picha za mradi**

### **1. Bwawa la Inala**



**Bwawa la Inala**

2. Wananchi katika mafunzo ya Mashamba Darasa ya Mpunga



3. Mashamba darasa ya Mpunga

